JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA UMMA

## FURSA YA KUONGEZA DALADALA - DAR ES SALAAM

***Dar es Salaam, 05 Novemba, 2025***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika hatua za kurejesha huduma za usafiri wa abiria kwa mabasi ya mjini yanayopita barabara ya Morogoro, sambamba na njia ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT - 1) Mkoani Dar es Salaam, inatangaza fursa za vibali vya muda kama ifuatavyo;

| NA | KUTOKA | KWENDA | KUPITIA BARABARA YA | UJAZO WA BASI KUANZIA ABIRIA | IDADI YA MAGARI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **MBEZI LUIS** | **MAKUMBUSHO** | **MOROGORO, KAWAWA , MWANANYAMALA** | **26** | **25** |
| 2 | **MBEZI LUIS** | **MNAZI MMOJA** | **MOROGORO** | **26** | **50** |
| 3 | **MBEZI LUIS** | **MUHIMBILI** | **MOROGORO** | **26** | **25** |
| 4 | **MBEZI LUIS** | **POSTA** | **MOROGORO, BIBI TITI, MAKTABA** | **26** | **50** |

- Huduma za daladala barabara ya Kilwa sambamba na BRT – 2 zitaendelea kwa mujibu wa leseni zilizotolewa

**Vigezo vya kuzingatia:**

1. **Vibali vitakavyotolewa ni kwa muda wa MIEZI MITATU, kuhuishwa kwake kutegemea hali ya huduma za usafiri wa abiria kwa Mabasi Yaendayo Haraka.**
2. Magari yatakayosajiliwa ni yenye usajili kuanzia namba **EJA**
3. Dereva wa gari husika awe amethibitishwa na LATRA

Digitally Signed By Salum PAZZY
Wed Nov 05 15:04:57 EAT 2025

Salum PAZZY

**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI YA VIBALI VYA MUDA**

1. Fungua mfumo wa **RRIMS** kupitia anwani: rrims.latra.go.tz
2. Fungua sehemu ya VIBALI (PERMIT) na uchague MAOMBI YA VIBALI (PERMIT APPLICATION)
3. Sehemu ya AINA YA OMBI (PERMIT TYPE) chagua ‘’Short Term’’
4. Sehemu ya SABABU (REASON) chagua Special Permit (BRT)
5. Sehemu ya Idadi ya siku andika 90 (Miezi mitatu)
6. Sehemu ya AINA YA ENEO LA SAFARI chagua ‘’Specific route’’.
7. Kisha endelea kwa kuchagua njia (route) unayohitaji katika njia zilizotangazwa.

Kwa maelezo Zaidi piga namba **0800110019** au **0800110020** au tuma barua pepe daressalaam@latra.go.tz